# Zana ya ukadiriaji wa uwezo wa uzingatiaji wa mgogoro

## Uwezo wa Shirika

### 1.1 Uwezo wa usimamizi na uongozi

Usimamizi/uongozi katika shirika unaelewa kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro na unaweza kufafanua kwa nini uzingatiaji wa mgogoro ni muhimu kwa shirika.

A. Wasimamizi wanafahamu kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro?

B. Wanaweza kufafanua kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro kwa usahihi?

C. Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro hupewa kipaumbele cha juu katika kufanya maamuzi?

D. Uwezo huo hujitokeza katika kufanya maamuzi yanayofaa, kutafuta nyenzo n.k?

E. Usimamizi umeendelea kuhimiza kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro ndani ya shirika na kwa washirika wa nje, wafadhili, n.k.?

### 1.2 Mbinu ya kukadiria wajibu na uwajibikaji

Mifumo ya kukadiria uwajibikaji ya shirika imewekwa ili kuwezesha kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro.

A. Mifumo iliyopo ya ufuatiliaji wa utendaji inazingatia mbinu za uzingatiaji wa mgogoro za wafanyakazi?

B. Kuna mfumo wa kuripoti ufuatiliaji wa mpango usiozingatia mgogoro?

C. Kuna mifumo ya kutoa zawadi ambapo uepukaji wa mipango isiyozingatia mgogoro unahimizwa kwa uwazi?

Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro imejumuishwa katika kigezo cha kufanya maamuzi kwenye michakato ya uidhinishaji wa mpango.

A. Kuna mbinu zozote za ukaguzi wa lazima wa hali ya uzingatiaji wa mgogoro kwenye mchakato wa uidhinishaji wa pendekezo la mpango?

B. Ni dhahiri kuhusu wanaowajibika na vipengele mbalimbali vya uzingatiaji wa mgogoro?

## Sera na mikakati

### 2.1 Sera ya uzingatiaji wa mgogoro

Kuna sera ya uzingatiaji wa mgogoro ya shirika au kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro imejumuishwa kwenye sera nyingine muhimu za shirika.

A. Kuna sera ya uzingatiaji wa mgogoro?

B. Mikakati au sera nyingine zozote muhimu za shirika zinarejelea kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro (kama vile mpango wa kimkakati wa miaka mingi au maadili bora)?

### 2.2 Sera na mikakati ya ndani

Sera/mikakati ya sasa mpango inalingana na sera ya uzingatiaji wa mgogoro.

A. Sera/mikakati muhimu ya mpango ya ndani ni ipi? (k.m.: Mkakati wa Mbinu Inayolingana na Haki, mkakati wa jinsia, mkakati wa ulinzi)

B. Sera hizi zinarejelea kwa uwazi kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro?

Sera za sasa za shirika zinalingana na sera ya uzingatiaji wa mgogoro.

A. Kuna sera za shirika zinazohusiana na kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro? (sera ya kupata nyenzo, sera ya uandikishaji wa watu, sera ya usafiri, sera ya ukaguzi, sera ya ushirikiano, sera ya usalama)

B. Sera hizi zinarejelea kwa uwazi kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro?

### 2.3 Sera na mikakati ya nje

Sera za sasa za nje ambazo shirika limeidhinisha zinalingana na sera ya uzingatiaji wa mgogoro.

A. Sera muhimu za nje ni zipi?

B. Sera hizi zinarejelea kwa uwazi kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro?

C. Kuna sera yoyote kati ya hizi inayoonekana kupinga kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro na inapaswa kuchunguzwa zaidi?

## Rasilimali watu – uwezo wa wafanyakazi, ujuzi na kuelewa kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro

### 3.1 Matarajio ya uzingatiaji wa mgogoro ya wafanyakazi

Shirika limebainisha matarajio (kuhusiana na vitendo mahususi) yanayotarajiwa kutoka kwa majukumu mbalimbali ya utendakazi ili shirika liweze kuzingatia mgogoro.

A. Matarajio ya kila jukumu kuhusiana na uzingatiaji wa mgogoro ni dhahiri?

B. Wafanyakazi wanafahamu athari za uzingatiaji wa mgogoro katika jukumu lao?

C. Wanapokea usaidizi wa kukuza ujuzi / ufahamu mahali ambapo kuna upungufu?

### 3.2 Uhamasishaji wa wafanyakazi kuhusu kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro, mtazamo na tabia

Wafanyakazi wana uwezo wa kutimiza matarajio ya kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro katika majukumu yao.

A. Wafanyakazi wanahisi kuwa wana uwezo wa kutimiza matarajio ya kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro katika majukumu yao?

Wafanyakazi wanaweza kuonyesha mitazamo na tabia zinazofaa.

A. Wafanyakazi wanafahamu mitazamo muhimu kuhusu kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro?

Mahali ambapo patatambuliwa kwamba kuna upungufu katika maarifa na ujuzi wa kisasa, shirika huhakikisha kuwa mafunzo yametolewa.

A. Kuna njia ya kimfumo ambapo mapungufu ya ujuzi/maarifa hutambuliwa na uwezo kukuzwa?

Shirika nzima lina ufahamu na hali ya kuelewa ya kiwango cha msingi kuhusu kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro.

A. Ni wafanyakazi wangapi ambao wanaweza kutoa ufafanuzi mzuri wa msingi kuhusu kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro na kwa nini ni muhimu kwa shirika?

B. Wafanyakazi wanaofanya kazi nje ya timu za mpango wanazingatia kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro kuwa muhimu kwa kazi yao? (k.m.: timu ya matangazo, fedha, utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa watu na vitu, rasilimali watu)

## Udhibiti wa mafunzo na maarifa

### 4.1 Mafunzo na mbinu ya kutafakari

Shirika lina udhibiti bora wa maarifa ya kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro, kurekodi na kujifunza kutokana na uzoefu wake katika kutumia kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro.

A. Mafunzo yaliyopatikana hukusanywa na kushirikiwa kwa njia gani?

B. Kuna zawadi gani zinazotolewa kwa watu ili washiriki maarifa yao ya mbinu duni za utekelezaji wa kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro?

Shirika limetengeneza 'mahali salama' ambapo watu wanaweza kuzungumzia kwa uwazi sehemu ambazo wanahisi kwamba mpango huenda ukasababisha athari mbaya kwa mgogoro.

A. Watu hufanya nini iwapo wanahisi kwamba mpango unaweza kuchangia kutokea kwa mgogoro?

B. Kuna mwongozo rasmi kuhusu hatua wanazopaswa kuchukua?

Shirika limekuza utamaduni wa kutafakari, ambapo kipaumbele cha kutosha hutolewa kwa kufikiria na kuchanganua, ambapo wafanyakazi huhimizwa na kuwezeshwa kufikiria kuhusu matokeo ya mpango yasiyotarajiwa ambayo yanaweza kujitokeza.

A. Kufikiria na kuchanganua hupewa kipaumbele kwa kiwango gani? Shirika huhakikishaje kwamba masuala kama hayo yamepewa kipaumbele?

### 4.2 Kuhimiza mbinu bora ya uzingatiaji wa mgogoro

Vikwazo vya kishirika vya uzingatiaji wa mgogoro vimekadiriwa na mfumo kuwekwa ili kuondoa vikwazo hivyo.

A. Shirika limezingatia kimfumo vikwazo vya uzingatiaji wa mgogoro (kabla ya ukadiriaji huu)?

B. Mabadiliko yoyote yamefanywa kutokana na hilo?

## Ujumuishaji katika hatua za mradi

### 5.1 Ujumuishaji katika usimamizi wa hatua za mradi/mpango

Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro imejumuishwa katika mifumo ya usimamizi wa hatua za mradi.

A. Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro imerejelewa katika mifumo ya usimamizi wa hatua za mradi, violezo na mwongozo?

B. Kuna mwongozo kuhusu iwapo kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro inapaswa kutumika kwa kina au la katika mikatadha mbalimbali?

C. Uzingatiaji wa mgogoro na matokeo yasiyotarajiwa kuhusu mgogoro ni sehemu ya lazima katika shughuli zote utathmini?

D. Majedwali ya mifumo wa kupanga vipengele muhimu vya mradi na uhusiano wake yana mgogoro pekee kama hatari kwa mradi (badala ya uhusiano wa pande mbili?)

Mifumo ya kufanya maamuzi inaweza kubadilika ili kuwezesha kufanywa kwa mabadiliko katika miradi kutokana na mabadiliko ya muktadha wa mgogoro.

A. Kuna mbinu na ujumbe dhahiri kwamba wakati shughuli zinatishia kuzidisha mgogoro wenye vurugu, shughuli hizo zitakaguliwa kama kipaumbele?

### 5.2 Ujumuishaji katika muundo wa mpango/mwanzo

Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro imejumuishwa katika muundo / pendekezo la mradi.

A. Uchanganuzi wa mgogoro ni sehemu ya lazima ya muundo wa mradi?

B. Wafanyakazi wanafahamu anayewajibika kwa kuangalia ikiwa uchanganuzi wa mgogoro umefanywa na kwa kuzingatia athari za uchanganuzi wa mgogoro kwa muundo wa mradi uliopendekezwa?

C. Wafanyakazi wanawajibika kwa uidhinishaji wa pendekezo la mradi kwa kuzingatia kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro?

D. Viashirio vya uzingatiaji wa mgogoro vimebuniwa?

Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro imejumuishwa katika mwanzo wa mradi.

A. Wafanyakazi wapya huelezwa mapema kuhusu kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro na kuhusu masuala ya mgogoro yanayohusiana na mpango wao?

### 5.3 Ujumuishaji katika mbinu ya ufuatiliaji na utathmini wa mpango

Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro imejumuishwa katika utekelezaji wa mradi.

A. Kuna kanuni ya kutafakari na kuripoti kila wakati kuhusu uhusiano kati ya mgogoro na mpango?

B. Wasimamizi / wafanyakazi nchini Uingereza huhimiza wasimamizi wa miradi / wafanyakazi wa ofisi ya nchini kushiriki kwa uwazi maelezo kuhusu matokeo mabaya yasiyotarajiwa ya mpango kwa njia gani?

C. Shirika huchocheaje hali ya kushiriki maelezo halisi ya matatizo ya mradi uliopo badala ya kushiriki habari za mafanikio pekee?

Vigezo vya utathmini vinajumuisha kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro.

A. Shughuli za utathmini huzingatia kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro ya mradi, hasa athari kubwa zisizotarajiwa?

B. Hali ya kuelewa kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro ni ya lazima wakati wa kuhoji / kuchagua washiriki?

### 5.4 Ujumuishaji katika utetezi wa haki, mawasiliano na kampeni

Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro hutumika katika utetezi wa haki, mawasiliano na kampeni.

A. Wafanyakazi wanaofanya kazi ya utetezi wa haki, mawasiliano na kampeni wanaona kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro kuwa muhimu kwa kazi yao?

### 5.5 Ujumuishaji katika huduma za usaidizi

Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro imejumuishwa katika rasilimali watu.

A. Mchakato wa makaribisho ya wafanyakazi unajumuisha kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro?

B. Ni maelezo gani ya kazi ambayo yanarejelea kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro kwa uwazi?

C. Mafunzo ya kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro yamejumuishwa katika maelezo ya kazi?

Ukaguzi unasaidia kwa ufanisi kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro.

A. Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro inachukuliwa kwa uzito kama masuala mengine ya usalama na fedha?

B. Wafanyakazi wa ukaguzi huzingatia kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro katika kazi yao?

Fedha huwezesha uzingatiaji wa mgogoro.

A. Idara ya fedha inaona kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro kuwa muhimu katika kazi yake?

Usalama na Mchakato wa Kupata Nyenzo huwezesha uzingatiaji wa mgogoro.

A. Idara ya usalama na mchakato wa kupata nyenzo inaona kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro kuwa muhimu katika kazi yake?

## Mahusiano ya nje

### 6.1 Wafadhili / ufadhili

Shirika hutoa maelezo ya wazi kwa wafadhili wote kwamba kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro ni ya lazima katika kazi yetu.

A. Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro inawasilishwaje kwa sasa kwa wafadhili?

B. Ni nafasi gani muhimu za kuzungumzia suala la uzingatiaji wa mgogoro na wafadhili?

C. Wakati mfadhili hayuko tayari kufadhili vipengele muhimu vya kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro (k.m.: uchanganuzi wa mgogoro), shirika hufanya bidii ya kutafuta nyenzo hizi mahali pengine au hukataa kufadhili vipengele hivyo au huchukua hatua nyingine?

Shirika huhakikisha kwamba nyenzo za kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro (muda wa wafanyakazi, ripoti ya mtaalamu panapohitajika, muda wa mpango wa kazi wa uchanganuzi wa mgogoro, nyenzo za uchanganuzi wa mgogoro n.k.) ni sehemu muhimu ya mapendekezo ya mradi.

A. Mapendekezo ya mradi hujumuisha: bajeti ya uzingatiaji wa mgogoro, muda wa uchanganuzi wa mgogoro kazini na viashirio vya uzingatiaji wa mgogoro?

### 6.2 Washirika

Kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro huzingatiwa na kupewa kipaumbele katika mahusiano na washirika.

A. Mwongozo wa uteuzi wa washirika unarejelea kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro?

B. Ni wakati na jinsi gani ambavyo tunaweza kuwaeleza washirika kuhusu matarajio yetu kuhusiana na suala la kanuni ya uzingatiaji wa mgogoro?

C. Tunawapa washirika usaidizi / mafunzo yoyote kuhusiana na uzingatiaji wa mgogoro?

D. Ni hatua gani itakayochukuliwa ikiwa mshirika atapatikana kwamba hazingatii mgogoro?